HOTUBA YA MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA, JAJI MKUU WA TANZANIA, KATIKA UFUNGUZI WA SIKU YA KIMATAIFA YA MAJAJI WANAWAKE, JOHARI ROTANNA HOTEL, DAR -ES -SALAAM - TAREHE 10.03.2024

Majaji wa Mahakama ya Rufani mliopo,

Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdalla, Jaji Mkuu wa Zanzibar,

Mheshimiwa Barke Sehel, Mwenyekiti wa Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake wa Tanzania (TAWJA) na Jaji wa Mahakama ya Rufani,

Majaji wa Mahakama ya Rufani mliopo

Majaji wa Mahakama Kuu Mliopo,

Majaji Wastaafu wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu mliopo,

Mhe. Imani Aboud, Jaji Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu,

Ndugu Peterson Magoola, UN Women Tanzania Representative,

Mhe. Balozi Mstaafu Mama Getrude Mongella,

Bi.Katarina Kuehn, Programme Manager, GIZ Tanzania

Waheshimiwa Wasajili na Naibu wasajili mliopo,

Mahakimu wa ngazi mbalimbali mliopo,

Viongozi mbalimbali wa Serikali mliopo,

Wafanyakazi wote wa Mahakama mliopo,

Wanachama wote wa TAWJA mliopo,

Waandishi wa Habari,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania!

Mahakama ya Tanzania! UADILIFU, UELEDI NA UWAJIBIKAJI!

SHUKRANI

1. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uzima, afya njema na kutupatia fursa hii ya kukusanyika leo hapa katika ukumbi wa Hotel ya Johari Rotanna kwa ajili ya hafla hii ya SIKU YA KIMATAIFA YA MAJAJI WANAWAKE (*The INTERNATIONAL DAY OF WOMEN JUDGES 2024*) kama ambavyo, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilivyoazimia Tarehe 28 Aprili 2021.

2. Aidha ningependa pia kutumia fursa hii ya pekee kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA) kwa kunipa

heshima ya kuwa mgeni rasmi katika Sherehe ya Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Majaji Wanawake.

3. Natumia fursa hii pia kuwashukuru uongozi mzima wa Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA) kwa juhudi zenu thabiti katika kuandaa Sherehe hii ya Siku ya Kimataifa ya Majaji Wanawake. Kusanyiko hili linadhihirisha mafanikio, mchango, na uthabiti wa wanawake katika kutoa haki kote ulimwenguni.

MAHAKAMA YA TANZANIA INAHESHIMU NA KUIENZI SIKU HII MUHIMU

4. Tovuti ya Umoja wa Mataifa kuhusu siku ya kimataifa ya Majaji Wanawake imebeba ujumbe maalum, *"To achieve Justice, we need more women in justice"*—Ili upatikanaji haki uwe kamilifu, wanahitajika wanawake wengi katika haki.
5. Siku ya leo, tarehe 10 Machi, 2024, ni siku mahsusi kukumbushana ukweli kuwa, uwakilishi wa kutosha wa wanawake katika ngazi zote za uongozi na maamuzi Mhimili wa Mahakama ndio njia pekee ya kuonyesha kuwa Mahakama zetu zina sura za wananchi na zinawakilisha

wananchi wake. Ni siku ya kutambua umuhimu wa Majaji na Mahakimu Wanawake katika kukuza utawala wa sheria, usawa. Pia ni siku ya kuwahimiza wanawake wengine na wasichana kutambua nafasi zao muhimu katika ustawi wa nchi zao na dunia kwa ujumla.

Aidha, Majaji na Mahakimu Wanawake mnapokutana tarehe 10 ya kila Mwezi Machi, ni siku ambayo sote tunazikumbusha Mihimili ya Dola umuhimu wa kuendelea kutunga sera, sheria na kuweka mikakati ya kuondoa vikwazo vinavyozuia maendeleo na ustawi wa wanawake.

6. Kwa upande wa Mhimili wa Mahakama, nina furaha kuona kwamba Siku ya Kimataifa ya Majaji Wanawake imekuwa ikipewa uzito na heshima na Wanawake wa Mahakama ya Tanzania tangu mwaka 2023 baada ya Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lililopitishwa tarehe 26 Aprili 2021 huko Doha Qatar.

Ni jambo la kupongeza Uongozi wa Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake wa Tanzania (TAWJA) kutujumuisha

leo, katika Mada itakayojadiliwa kuhusu—"**Mwanamke katika Utoaji Haki: Tafakuri ya Msongo wa Mawazo na Majukumu ya Kijinsia.**" Hii ni nafasi kwetu tutafakari kwa kina, suala msongo wa mawazo unavyoweza kuathiri nafasi na mchango muhimu wa Majaji na Mahakimu Wanawake katika utoaji haki.

UTHIBITISHO KUWA MAJAJI NA MAHAKIMU WANAWAKE NI NGUZO INAYOTEGEMEWA NA MHIMILI WA MAHAKAMA KATIKA UTOAJI HAKI

7. Hapana shaka yoyote kuwa Takwimu zinathibitisha mchango mkubwa wa wanawake katika mifumo yetu ya Mahakama.

Uzoefu wetu kila siku Mahakamani, tumeona mchango wa Majaji na Mahakimu Wanawake. Wanawake wanasimama kama walinzi wa sheria na taa ya usawa, huruma, imani na hekima. Wanaleta meza ya mtazamo chanya, ufahamu, na uzoefu tofauti, uwiano wa kisheria na kukuza jamii inayoshirikishwa zaidi na yenye usawa.

8. Jaji Sandra Day O'Connor (aliyefariki tarehe 1/12/2023), alikuwa Jaji wa Mwanamke wa Kwanza kuteuliwa mwaka 1981 katika Mahakama ya Juu ya Marekani *(Supreme Court)*. Jaji huyu aliwahi kuandika kuwa uwepo wa Majaji Wanawake ndani ya Mhimili wa Mahakama una matokeo chanya zaidi ya idadi yao au idadi ya mashauri wanayosikiliza *(multiplier effect)*:

"The multiplier effect is the notion that investing in women and girls not only has a positive impact on the women and girls themselves, but also on their families and the societies in which they live. Women's participation in the judiciary may be of particular importance in the implementation and enforcement of laws that allow for women's full participation in society. Women's presence in the judiciary system enhances the legitimacy of courts and sends a powerful message saying that they're open and accessible to those who want to seek justice."

9. Nawaomba Majaji na Mahakimu wanawake endeleeni kuwa mwanga unaohamasisha wanawake wengine na wasichana

kutambua wana nafasi na wana mchango katika mfumo wa utoaji haki na utawala wa sheria Tanzania na Duniani kote.

10. Jaji wa Rufani Mstaafu Eusebia Munuo ni mfano, mwanga na Ushahidi tosha wapi Majaji na Mahakimu wametoka, na umbali uliopo mbele yetu kufikia mizani ya usawa.

11. Takwimu za Mahakama ya Tanzania kuhusu uwakilishi wa wanawake katika ngazi mbalimbali inaonyesha hatua kubwa iliyofikiwa na pia safari ndefu iliyo mberle yetu. Hadi tarehe 08/03/2024 takwimu zinaonyesha uwepo wa wanachama wa TAWJA katika ngazi za Mahakama kama ifuatavyo;

***Idadi ya Majaji Mahakama ya Rufani Majaji* 35**	Majaji wa Rufani (Wanaume-**22**)	Majaji wa Rufani (Wanawake-**13**)	Asilimia: Wanawake-**37%** Wanaume-**63%**
***Idadi ya Majaji Wafawidhi*-26**	Majaji Wafawidhi (Wanaume-**17**)	Majaji Wafawidhi (Wanawake-**9**)	Asilimia: Wanawake-**35%** Wanaume- **65%**

***Idadi ya Majaji wa Mahakama Kuu Majaji* 105**	(Wanaume-**67**)	(Wanawake-**38**)	Asilimia: Wanawake-**36%** Wanaume-**64%**
***Wasajili*- 1**	(Wanaume- **1**)	(Wanawake-**0**)	Asilimia: Wanawake-**0%** Wanaume-**100%**
***Manaibu Wasajili*- 78**	(Wanaume-**40**)	(Wanawake-**38**)	Asilimia: Wanawake-**49%** Wanaume-**51%**
***Mahakimu Wakazi*- 1,126**	(Wanaume-**567**)	(Wanawake-**559**)	Asilimia: Wanawake-**50%** Wanaume-**50%**
***Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo*- 229**	(Wanaume-**134**)	(Wanawake-**95**)	Asilimia: Wanawake-**41%** Wanaume-**59%**

12. Pia juhudi zimeendelea kufanyika kwa kuhakikisha usawa wa kijinsia unapewa kipaumbele kwa kuajiri wafanyakazi wa Mahakama katika kada nyingine ambapo katika majukumu

ya utawala, wanawake wanachukua 14% ya nafasi za Wakurugenzi na 50% ya nafasi za Wakurugenzi Wasaidizi na kushikilia uwakilishi mkubwa katika majukumu mbalimbali mengine, kama vile maafisa utumishi na maafisa tawala.

13. Nawapongeza Majaji na Mahakimu Wanawake kuwa asilimia za uwepo wenu katika ngazi na nafasi mbalimbali zinatokana na uwezo wenu, na sio asilimia za upendeleo.

PONGEZI KWA KUCHAGUA MADA—"MSONGO WA MAWAZO NA MAJUKUMU YA KIJINSIA"

14. Baada ya kupokea ratiba ya leo, nilimpongeza Mwenyekiti wa TAWJA kwa kuchagua mada katika eneo jipya kwetu, ambalo Mhimili wa Mahakama haujajifanyia utafiti na kujitathmini.

15. Dr. Joseph Sadek, Mental Health Advisor of the Caribbean and Commonwealth Judicial Institute aliwahi kuandika: ***"Wellbeing of Judges should be a priority for every Judiciary."*** Alifafanua: *"The term wellbeing encompasses both personal wellness and professional wellness, including job satisfaction, engagement and reduced burn-out. It is*

closely linked to quality of life as a broad term comprising domains of physical health, psychological state, social relationships and environment."[1]

16. Msongo wa Mawazo *(mental stress)* na majukumu ya kijinsia ni mambo ambayo yanaweza kuathiri ushiriki kamilifu wa Majaji Wanawake katika ngazi zote za Mahakama.

Ningependa kuwasihi viongozi wa TAWJA kuwa, wakati umefika wa kufanya utafiti wa kina kuhusu athari ya Msongo wa Mawazo kwa Majaji na Mahakimu wanawake Tanzania.

17. Mwandishi mmoja aitwaye Chris Aupperle aliandika Makala kuhusu utafiti uliofanywa huko Marekani kuhusu Msongo wa Mawazo unaowakabili Majaji wa Marekani. Ingawa utafiti huo haukujikita kwa kuangalia msongo wa Mawazo miongoni mwa Majaji Wanawake, utafiti huo unatoa picha ya stress Majaji wanazokutana nazo wakiwa kazini.

[1] United Nations Office on Drugs and Crime (UNODC), unodc.org

Utafiti uliwashirikisha Majaji zaidi ya elfu moja, na uliitwa usongo wa Mawazo na ustahimilivu wa usongo huo ndani ya Mhimili wa Mahakama huko Marekani *(Examining Stress and Resiliency Within Our Judiciary).* Naamini leo hii, mtapata muda wa kujadili pia mbinu mbali mbali za kukabiliana na msongo, na kuzistahimili.

18. Ili kubaini mambo yanayosababisha msongo wa mawazo kwa Majaji, watafiti waliwaomba majaji waliododoswa waorodheshe visababishi 37. Sababu mbili zilizotajwa na wengi zilikuwa msongo utokanao na matokeo ya maamuzi yao *(the impact of their decisions)* na mzigo mzito wa mashauri unaobebwa na kila Jaji *(heavy caseload)*.

19. Sababu nyingine zilizotajwa kusababisha msongo wa Mawazo zilitokana na mkutaniko baina ya Majaji kwa upande mmoja, na wadaawa na wadau wa Mahakama, kwa upande wa pili.

Sababu hizi ni pamoja na Mawakili wanaendesha mashauri bila matayarisho ya kutosha (Nafasi ya 3); Wadaawa wanaojiwakilisha wenyewe bila msaada wa mawakili (Nafasi

ya 4); Wadaawa wanaojiwakilisha wenyewe hujikita kwenye mambo ambayo hayausiani na mgogoro ulio mahakamani (nafasi ya 5);

Msongo wa Mawazo kutokana na mashauri yanayohusu migogoro baina au miongoni mwa wadaawa wa familia moja kwa mfano kugombea mali au matunzo ya Watoto. Sababu zingine ambazo huwapa Majaji msongo wa Mawazo ni wananchi wengi kutoelewa namna Mahakama zinavyofanya kazi;

kesi zinazotokana na ukatili wa kupindukia na kuongezeka kwa Mawakili wasio na adabu au wasio waadilifu pia huwaongezea Majaji msongo mkubwa wa Mawazo.

20. Waliowatafiti wa Majaji wa Marekani waliainisha pia athari za msongo wa Mawazo zilizowakabili Majaji. Majaji wengi zaidi walitaja msongo wa Mawazo huwasababishia uchovu wa kimwili *(fatigue)*.

Nafasi ya pili ni kupata usingizi kwa taabu *(sleep disturbance)*. Athari nyingine zilizotajwa na majaji wa

Marekani ilikuwa— hofu kuhusu afya zao; na kukosa amani binafsi. Wakati mwingine Jaji hufikiria yeye ni mgonjwa, kumbe ni msongo wa Mawazo.

21. Majaji wa Marekani waliainisha hatua mbalimbali *(resiliency)* wanazochukua kukabiliana na msongo wa Mawazo. Kujichanganya na kushirikiana na majaji wenzako katika shughuli za kijamii, ilitajwa na Majaji wengi kama mbinu ya kwanza kukabiliana na msongo wa Mawazo. Wengine hutegemea nasaha kutoka kwa Majaji wenzao wanaowaamini.

22. Kufanya mazoezi kulitajwa na Majaji wengi kama njia ya kukabiliana na msongo wa Mawazo. Wengine walitaja kula chakula bora, ibada na kupata usingizi wa kutosha, ni njia zingine za kukabiliana na msongo wa Mawazo.

23. Utafiti wa Majaji wa Marekani haukujikita msongo wa mawazo unaowakabili Majaji wanawake kazini na wakiwa nyumbani baada ya kazi. Matarajio ya kijamii na tamaduni

zinazohusiana na jinsia zinaweza kusababisha msongo wa mawazo kwa wanawake katika utoaji haki.

Tunaposherehekea hatua zilizopigwa katika kuendeleza haki ya kijinsia ndani ya Mahakama, lazima pia tufanye utafiti wa kina kuhusu changamoto zinazowakabili Majaji Wanawake katika mfumo dume wa kijamii na kiutamaduni ambao huchangia msongo wa mawazo na kuwaathiri sana wanawake katika taaluma ya kisheria na utoaji haki.

24. Majaji na Mahakimu Wanawake wanakabiliwa na changamoto nyingi zinazotokana na mila na desturi za kibaguzi ndani ya jamii. Jambo linalowalazimu kupambana na majukumu ya kazi, maisha yao binafsi, na familia, wakikabiliwa na dhana potofu juu ya uwezo wao kitaaluma na viwango vya kutekeleza majukumu yao. Hali ya asili inayovuta hisia za kazi zao mara nyingi husababisha uchovu, ikichangiwa na matarajio kuhusu utunzaji wa watoto na majukumu ya nyumbani.

HITIMISHO—Tuitumie Siku ya Leo kutafakari na kutathmini Safari ya Jaji na Hakimu Mwanamke Tanzania

25. Siku ya Kimataifa ya Majaji Wanawake ni fursa ya kusherehekea mafanikio ya wanawake katika haki na kujenga ajenda ya usawa wa kijinsia katika mfumo wa Mahakama. Huu pia, ni wakati wa kuonyesha umuhimu wa uwakilishi wa kijinsia katika uongozi wa kisheria na kujitolea kwa wanawake katika kutoa haki na usawa.

    Siku ya leo ni siku yenu kukusanya mrejesho kwa Uongozi wa Mahakama kuhusu maeneo yenye changamoto zinazowakabili Majaji na Mahakimu Wanawake yanayohitaji maboresho.

26. Baada ya kusema hayo machache, sasa ninayo furaha tele kutangaza kuwa kongamano la Siku ya Kimataifa ya Majaji Wanawake limefunguliwa rasmi.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA!